

Kongamano hilo lenye kaulimbiu 'Ushirikiano wenye Usawa kwa Maendeleo Jumuishi na Endelevu',

wa makubaliano baina ya TIC na Baraza la Biashara la Uholanzi na Afrika (NABC) utachangia kuon-

za biashara na uwekezaji na kuimarisha ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

# HABARI LEO UK 5 Vijana BBT-Life wahimizwa fursa kupunguza tatizo la ajira

Na Upendo Masha, Bagamoyo

**V**IJANA wanufaika wa Programu ya mradi wa Kielelezo, Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT – Life), wametakiwa kufanya vizuri kwa kutumia fursa waliyopata, hatua itakayosaidia lengo la serikali la kupunguza tatizo la ajira nchini kufanikiwa.

Wito huo ulitolewa na Mwekezaji na Mkurugenzi wa Ranchi ya Mbogo, Naweed Mulla, wakati akizunguma na vijana zaidi ya 45 kutoka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TAWIRI) na Chuo cha Mifugo Buhuri Tanga, waliofika katika ranchi hiyo kwa

ajili ya mafunzo kwa njia ya vitendo katika Kata ya Ubena, Halmashauri ya Chalinze, wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani.

Naweed alisema serikali imetoa fursa kwa vijana hao kushiriki katika mradi huo hivyo ni wajibu wao kuhakikisha wanazingatia yale yote waliyofundishwa na kuwa na nidhamu na maadili hatua itakayosaidia kuleta mapinduzi chanya katika sekta ya ufugaji bora wenye tija nchini.

Naweed ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha wafugaji Kibiashara nchini, alitoa wito kwa wawekezaji wengine binafsi kuona umuhimu wa kuunga mkono jitihada za serikali katika kutoa elimu kwa vijana wana-

okusudia kuingia katika sekta hiyo kwa maslahi ya uchumi wa taifa.

Mkufunzi wa wanafunzi hao kutoka chuo cha mifugo Buhuri, Tanga, Joseph Moshi alisema lengo la mradi huo ni kuwapa vijana mafunzo, uzoefu, ujasiri katika kubuni na kuendesha miradi ya ufugaji katika unenepeshaji wa mifugo kibiashara kwa ajili ya kuongeza tija na faida mara dufu.

Baadhi ya vijana hao, walisema wamepata manufaa makubwa kushiriki mafunzo hayo kwa njia ya vitendo na kwamba wamekuwa namna ya kunenepesha mifugo na kufanya biashara hiyo kwa tija zaidi tofauti na ilivyokuwa awali.

Ucnumi wa Kijani na Mazingira wa Zambia, Dk Collins Nzovu. Mkutano huo ulifanyika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Mulungushi, Lusaka, Zambia juzi. (Picha na Ofisi ya Makamu wa Rais).

HABARI LEO UK 7

# Mifugo yaingizwa kinyemela Hifadhi ya Ruaha\*

Na Joachim Nyambo,  
Ruaha

**M**IFUGO 345 ikiwemo ng'ombe, mbuzi na kondoo imekamatwa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ikiwa imeingizwa na wafugaji kinyume cha sheria.

Imeelezwa kuwa mifugo hiyo imekuwa ikiingizwa usiku na mapema asubuhi hutolewa hifadhini humo.

Pia trekta moja limekamatwa ndani ya hifadhi hiyo

ambapo kukamatwa kwa mali hizo zote kunatokana na doria iliyofanywa na askari wa uhifadhi wakati wakitekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria ya Hifadhi za Taifa Tanzania Sura ya 282 marejeo ya mwaka 2002.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi, Godwell Meng'ataki, mifugo hiyo 345 ilikamatwa Novemba 13 na 14, mwaka huu ikiwa zaidi ya kilometa 100 kutoka eneo ulipo

mpaka.

Meng'ataki alisema mifugo hiyo ilikutwa ndani ya eneo oevu lililopo ndani ya hifadhi hiyo litumikalo kutunzia maji na pia kuzalisha maji kwa ajili ya Mto Ruaha.

Alisema wafugaji hao wamebuni mbinu ya kuingiza mifugo usiku wa manane na kuiondoa alfajiri jambo linalo lazimu askari kutumia mbinu nyingi kuwakamata.

Meng'ataki alisema kwa upande wa trekta lilikutwa likitumiwa na majangili walio

ingia eneo hilo na kulitumia kulima pasipo kujali kuwa eneo husika ni sehemu ya hifadhi na hawaruhusiwi kufanya shughuli za kibinadamu ikiwemo kilimo.

Alisema maofisa na askari wa Hifadhi ya Taifa Ruaha wameendelea kukabiliana na vitendo vya ujangili ndani ya bonde la Ihefu ili kuhifadhi vyanzo vya maji kwa ajili ya "The Great Ruaha" na bioanuai zilizomo katika hifadhi hiyo ya pili kwa ukubwa Tanzania kwa ajili ya maendeleo ya utalii na